KELIN
Reclaiming Rights, Rebuilding Lives



# Usajili wa Ndoa

Kijitabu hiki cha Usajili wa Ndoa ni dira ya kukusaidia kujua na kufahamu vyema namna ya kusajili na kuhalalisha ndoa yako. Kijitabu hiki kitakuarifu kuhusu stakabadhi unazohitaji na utaratibu unaohitaji kufuata kuhakikisha kuwa ndoa yako inatambuliwa kwa mujibu wa Sheria.

Uimarishaji Uwezo Kiasasi na KELIN Kenya

©2020 KELIN

Haki zote zimehifadhiwa. Hakuna sehemu ya kitabu hiki inayoweza kutoleshwa au kutumiwa katika umbo lolote lile au kwa njia nyingine bila kibali cha mchapishaji.

# Maana ya ndoa

Ndoa ni ushirikiano wa kujitolea baina ya mwanamume na mwanamke ama katika ndoa ya mke/mume mmoja au ya kimitala (wake zaidi ya mmoja) na ambayo imesajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Ndoa. Wanaooana lazima wawe watu waliofikisha umri wa miaka kumi na minane, kuwa na haki sawa na haja wakati huo, katika ndoa na wakati wa kuvunjilia mbali ndoa.



# Aina za Ndoa

Ndoa inaweza kusajiliwa iwapo inasherehekewa kama ndoa ya kitamaduni, kiraia au kidini.

## a) Ndoa za Kitamaduni

Ndoa hizi husherehekewa kwa mujibu wa utamaduni wa jamii ya mmoja wa au wote wawili wanaonuia kushiriki katika ndoa husika. Lazima pawepo na malipo ya aina fulani kama vile pesa, malipo ya mwanzo au mahari ili kuhalalisha ndoa kama hiyo.

Baada ya kukamilisha vizuri hatua mahususi zinazohitajika ili kuidhinisha hali ya ndoa kama hiyo, wanaoona hutuma notisi kwa msajili wa ndoa kuhusu usajili. Kwa vile ndoa za kitamaduni zina uwezo wa kubadilika kuwa za kimitala (za wake wengi), ndoa zote baina ya mwanamume na kila mke wake lazima zisajiliwe kila moja kivyake kwa minajili ya utoaji cheti cha ndoa.

## b) Ndoa za Kiraia

Ndoa hizi husherehekewa na Msajili wa ndoa. Mara nyingi ndoa hizi ni za mke/mume mmoja k.v. mtu hawezi kuoa zaidi ya mke mmoja. Wanaonuia kuoana lazima wampe Msajili notisi ya nia yao ya kuoana. Yeyote aliye na pingamizi anaweza kuliwasilisha kwa Msajili wa ndoa.

## c) Ndoa za Kikristo

Ndoa hizi zinahusisha watu wanaofuata imani ya Ukristo. Zinasimamiwa na mhubiri mkuu wa kanisa aliyeidhinishwa ambaye baadaye humpelekea msajili cheti ili kusajiliwa.

## d) Ndoa za Kihindi

Ndoa hizi zinahusisha watu wanaofuata imani ya Kihindi. Ndoa hizi zinaweza kusimamiwa na msajili wa ndoa au mtu yeyote aliyekubaliwa kwa mujibu wa itikadi za dini ya Kihindi za wanaoshiriki katika ndoa. Anayesimamia ndoa hiyo hurekodi habari kuhusu ndoa hiyo na kumkabidhi msajili rekodi hiyo ili kusajiliwa.

## e) Ndoa kwa mujibu wa sheria za Kiislamu

Ndoa hizi zinahusisha watu wanaofuata imani ya Kiislamu na husimamiwa na Kadhi, Sheikh au Imamu aliyekubaliwa na Msajili wa ndoa. Anayesimamia ndoa hiyo hurekodi habari kuhusu ndoa hiyo na kutoa cheti cha ndoa. Baadaye hupeleka rekodi hiyo na kuidhinisha cheti kwa minajili ya kusajiliwa.



## Mashahidi wa Ndoa

Ndoa iliyofanyika kwa mujibu wa Sheria ya Ndoa lazima iwe na mashahidi wawili waliohitimu ambao lazima watosheleze mahitaji yafuatayo:

- wamefikisha umri wa miaka kumi na minane;
- wana akili timamu;
- sio mlevi hadi hawezi kuelewa wanachofanya wanaoana;
- wana uwezo wa kuelewa lugha inayotumiwa katika sherehe ya ndoa; na
- sio yule anayesimamia sherehe hiyo ya ndoa

## Kipindi cha Kudumu kwa Ndoa

Ndoa iliyosajiliwa kwa mujibu wa Sheria hudumu hadi itakapoamuliwa na:

- kifo cha mke/mume;
- mahakama kutangaza kutosheka na hali ya kifo cha mke/mume;
- kubatilishwa au kutengana.

## Kanuni za Ndoa za Kitamaduni

Usajili wa ndoa za kitamaduni nchini Kenya hulindwa na Ndoa (Ndoa ya Kitamaduni) Kanuni 2017, chini ya Sheria ya Ndoa. Kanuni hizi ziliidhinishwa katika Notisi ya Gazeti Nambari 5345 iliyotolewa tarehe 9 Juni, 2017. Notisi hiyo ilitaka kuwa ndoa zote za kitamaduni zisajiliwe kutokea tarehe 1 Agosti, 2017.

## Mahitaji ya Usajili

Ili ufaulu katika shughuli za usajili wa ndoa ya kitamaduni nchini Kenya, unahitaji stakabadhi zifuatazo:

- Kila mmoja lazima alete picha yake moja ya pasipoti.
- Kila mmoja lazima awe na cheti cha kuzaliwa au stakabadhi inayotangaza umri wa kila mmoja wao.
- Kila mwombaji lazima awe na stakabadhi za kumtambulisha.
- Kila mmoja lazima awasilishe cheti au barua ya kumtambulisha kutoka kwa chifu.

# Utaratibu wa Usajili

**HATUA 01**

Wote kushiriki katika itikati za kitamaduni kulingana na jamii zao;

**HATUA 02**

Kumuarifu msajili wa ndoa katika kipindi cha siku 90 kuhusu nia yao ya kusajili ndoa yao kwa kujaza fomu inayolipiwa ada;

**HATUA 03**

Msajili huweka notisi ya siku kumi na nne ya kuyaomba mapingamizi kutoka kwa watu ambao wanaweza kupinga ndoa hiyo;

**HATUA 04**

Iwapo kuna mapingamizi, malalamiko hupokelewa, husikizwa na kuamuliwa;

**HATUA 05**

Iwapo hakuna mapingamizi yaliyotolewa au yameshughulikiwa, basi msajili atawakabidhi wanandoa hao cheti cha kukubaliwa kwa kulipa ada;

**HATUA 06**

Watu hao wawili lazima watume ombi la usajili wa ndoa yao pamoja na nakala ya cheti cha kukubaliwa kutoka kwa msajili kwa kulipa ada;

**HATUA 07**

Msajili akiridhika na ombi lao na kufanya uchunguzi husika, basi hutoa cheti cha ndoa.



## Kuvunjiliwa kwa Ndoa

Hiki ni kitendo au mfanyiko wa kuvunjiliwa mbali kwa ndoa kwa mujibu wa sheria. Ndoa inaweza kuisha kutokana na sababu zifuatazo:

- Uzinzi;
- Ukatili;
- Utelekezi;
- Unyimaji kupita kiasi;
- Kutoshirikiana kusikorekebishika katika ndoa;
- Sababu yoyote halali kwa mujibu wa sheria ya kitamaduni ya mshtaki;
- Kubadilisha dini tofauti kwa mujibu wa Kihindi

KELIN

Reclaiming Rights, Rebuilding Lives

**OFISI YA NAIROBI**
Karen C, Njia ya Kuwinda,
Kutoka Barabara ya Lang'ata
S.L.P. 112 - 00202, KNH Nairobi
Simu: 020 2515790
Rununu: 0710 261408 / 0788 220300
Kipepesi: 020 386 1390

---

**OFISI YA KISUMU**
Mtaaa wa Nyalenda Railways ,
Bloku 9/220, Karibu na Barabara ya Nairobi,
Mkabala wa YMCA
S. L.P. 7708 - 40100 Kisumu - Kenya
Simu: +254 57 204 1001